# Ubepari Umeunda Janga la Mabadiliko ya Tabia Nchi; Usoshalisti Unaweza Kuiondoa Dhahma Hiyo. Jarida la Thelasini na Tano (2022)



George Bahgoury (Egypt), *Untitled*, 2015.

Marafiki wapendwa,

Salamu toka dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.

Mwezi Novemba,mwaka huu 2022,mataifa mengi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) watakusanyika katika jiji la kitalii la Sharm El Sheikh nchini Misri kwaajili ya mkutano wa mwaka wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi. Huu ni mkutano wa 27 wa wadau wa kuangazia Mpango Kazi wa UN wa Mabadiliko ya Tabia Nchi, ukifahamika kama COP 27.

Makubaliano ya kimataifa ya mazingira yaliasisiwa huko Rio de Janeiro mwaka 1992, huku mkutano wa kwanza ukifanyika Berlin mnamo mwaka 1955; maazimio yalitanuliwa zaidi katika Itifaki ya Kyoto ya mwaka 2005 na yakasisitizwa zaidi katika Makubaliano ya Paris ya mwaka 2015.Hakuna la ziada linalohitajika kusemwa kuhusu janga la tabia nchi linalohatarisha kuangamia kwa viumbe wengi. Kuondoka kutoka nishati ya ukaa kumeshindika kutokana na vikwazo vitatu:

1. Kani za mrengo wa kulia zinazokataa uwepo wa mabadiliko ya tabia nchi.
2. Sehemu ya wadau wa nishati wenye maslahi na kuendelea kwa nishati-ukaa.
3. Kukataa kukubali kwa mataifa ya magharibi kuwa mataifa yao ndio wahusika-msingi wa tatizo lililopo na kugomea kuwajibika kufidia kwa kukataa kuukimu mchakato wa mabadiliko ya nishati katika mataifa yanayoendelea, mataifa ambayo wanaendelea kunyonya utajiri wake hata sasa.

Katika mijadala ya wazi juu ya dhahma ya tabia nchi, kuna rejea chache kuhusu Mkutano wa Ulimwengu wa Rio wa mwaka 1992 na mkataba uliosema: ‘Ukubwa wa suala la mabadiliko ya tabia nchi unalazimisha ushirikiano mpana kadiri iwezekanavyo kwa mataifa yote na ushiriki wao katika jitihada madhubuti za kimataifa, kwa kuzingatia majukumu na uwezo kwenye malengo yanayofanana pamoja na hali za kiuchumi na kijamii’. Ni katika kutambua hoja kuwa kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabia nchi ni lile lile kwa nchi zote na hakuna nchi yenye kinga ya madhara yake, lakini uhusika wa nchi katika kusababisha tatizo, hakupo sawa. Baadhi ya nchi ambazo zimenufaika na ukoloni na nishati-ukaa kwa karne nyingi zina wajibu mkubwa zaidi katika kuondoa matumizi ya nishati ukaa katika mfumo ya nishati.



Roger Mortimer (Aotearoa/New Zealand), *Whariwharangi*, 2019.

Hoja ya kitaaluma juu ya hili,ipo bayana: Mataifa ya magharibi yalinufaika na ukoloni na nishati-ukaa katika kufikia ngazi waliyonayo sasa kimaendeleo. Takwimu kutoka Global Carbon Project, iliyoongozwa na Kituo cha Uchambuzi wa Taarifa za Kaboni Dayoksaidi ambacho sasa hakifanyi kazi na kilichokuwa chini ya wizara ya nishati ya Marekani zinaonyesha kuwa Marekani kwa kiwango kikubwa ndiye mzalishaji mkubwa wa hewa ya ukaa tangu mwaka 1750. Marekani pekee , imezalisha zaidi hewa ya ukaa kushinda Umoja wa Ulaya, mara mbili zaidi ya China, mara nane zaidi ya India. Wazalishaji wakubwa wa hewa ya ukaa walikuwa mataifa yote ya

kikoloni, Marekani,Ulaya,Canada na Australia, licha ya kuwa na moja ya kumi ya idadi ya watu wa ulimwengu mzima pekee, yanawajibika kwa kuzalisha zaidi ya nusu ya hewa ya ukaa tangu karne ya 18, mataifa haya si tu yamemwaga hewa ya ukaa huko hewani, lakini yanaendelea kuongeza ngwe zao katika uzalishaji wa hewa ukaa.

Ubepari unaoendeshwa kwa nishati- ukaa , ulionawirishwa na utajiri ulioporwa nyakati za ukoloni, umeiwezesha Ulaya na Marekani ya Kaskazini kuimarisha ustawi wa watu wake kufikia maendeleo ya hali ya juu kabisa. Hali ya juu ya kutokuwepo usawa katika viwango vya maisha baina ya mtu wa kawaida wa Ulaya (ambao wapo watu 748 milioni) na mtu wa kawaida wa India (ambao wapo watu bilioni 1.4) ni mara saba zaidi sasa kuliko ilivyokuwa karne moja iliyopita. Ingawa utegemezi wa China, India na mataifa mengine yanayoendelea kwa nishati ya ukaa hususani makaa ya mawe umeongezeka, kufikia kiwango cha juu, kiwango cha uzalishaji hewa ya ukaa kwa mtu mmoja mmoja kimeendelea kusalia kidogo kulinganisha na Marekani, ambayo kiwango cha uzalishaji hewa ya ukaa kwa mtu mmoja ni takribani mara mbili zaidi ya China na mara nane zaidi kushinda kile cha India.

Upungufu wa utambuzi wa ubeberu wa tabia nchi unapelekea kushinda kuendesha Mfuko wa Tabia Nchi ya Kijani, ambao uliundwa mwaka 2010 katika COP 16 ukiwa na lengo la kusaidia mataifa yanayoendelea kuondokana na maendeleo ya kijamii yenye kutegemea nishati-ukaa.




Katika ngazi ya kiulimwengu, mjadala juu ya namna gani ya kushughulikia janga la tabia nchi mara nyingi umezunguka katika namna nyingi za Mkataba Mpya wa Kijani (Green New Deal), kama vile European Green Deal, North American GND, na Global GND, ambayo yanaungwa mkono na mataifa (serikali mbalimbali), mashirika ya kimataifa, na mavuguvugu fulani fulani ya mazingira. Ili kuelewa vema na kuimarisha mjadala ofisi ya Tricontinental: Institute for Social Research huko Buenos Aires, Argentina, ilikusanya wanazuoni wa-ikolojia nguli kuangazia GND mbalimbali na kutizama juu ya uwezekano kuyafikia mageuzi ya kuondoa dhahma ya tabia nchi. Mjadala ule na José Seoane (Argentina), Thea Riofrancos (United States), na Sabrina Fernandes (Brazil) -ambao kwa sasa upo katika notibuku namba 3 (Agosti 2022), " *The Socioenvironmental Crisis in Times of the Pandemic: Discussing a Green New Deal*".

Wanazuoni hawa watatu wanatoa hoja kuwa ubepari hauwezi kutatua janga la mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwa ubepari ndio sababu msingi ya uwepo wa janga hilo.  Makampuni makubwa mia moja kati ya makampuni makubwa ulimwenguni yanachangia 71% ya hewa chafu za viwandani (kwa kiasi kikubwa hewa ya ukaa ya kabonidayoksaidi na methane); makampuni haya yakiongozwa na viwanda vya nishati ukaa ,hayakubali kuongeza jitihada za mageuzi ya nishati licha ya kuwa na uwezo wa kiteknolojia wa kuweza kuzalisha mara kumi na nane ya mahitaji ya

umeme ya ulimwengu mzima kwa umeme wa upepo pekee. Uendelevu, neno ambalo limeondolewa kabisa maudhui yake halisi katika mazungumzo na mijadala mingi, si neno lenye kuleta faida kwa makampuni haya.

Kwa mfano, mradi wa kijamii wa nishati-rejea (renewable) ,hautazalisha faida kubwa kwa makampuni makampuni ya nishati za fosili. Maslahi kutoka kwa kampuni fulani fulani za kibepari katika GND zikihamasishwa vilivyo na usongo wao wa kuzivuna fedha za umma ili wandelee kuunda uhodhi binafsi kwa maslahi ya tabaka la kibepari linalomiliki makampuni makubwa yanayochafua na kujaribu mazingira ya ulimwengu.

Ila, kama Riofrancos afafanuavyo katika notibuku, “Ubepari wa kijani” unakusudia kuondoa tu dalili za ubepari nfano – kuongezeka kwa jotoridi ulimwenguni, kuangamia kwa viumbe wengi, kuharibiwa kwa mfumo wa kiikolojia –bila Kufanya mageuzi katika miundo ya ulimbikizaji na matumizi ndiko kumepelekea janga la tabia nchi. Ni **“techno-fix”**: vichekesho vya kubadili vyote bila kubadili chochote ’.



Gonzalo Ribero (Bolivia), *Ancestor*, 2016

Mjadala juu ya GNP unaibuka, kama Seoane anavyoonesha, kutoka katika hatua mbalimbali kama zile za ripoti ya amani ya mwaka 1989,*iliyo Msingi wa Uchumi wa Kijani, ambayo iliandaliwa kwaajili ya serikali ya Uingereza na kupendekeza matumizi ya fedha za umma katika kuunda teknolojia mpya kwa makampuni binafsi* kama suluhu ya majanga yanayokabili chumi za magharibi. Dhana ya *'uchumi wa kijani'* haikuwa kwaajili ya kuufanya uchumi kuwa wa 'kijani', isipokuwa kuitumia dhana ya 'umazingira' kuimarisha ubepari. Mwaka 2009, wakati wa mdodororo wa uchumi wa ulimwengu, Edward Barbier, mwandishi-mwenza wa Ripoti ya Amani, aliandika ripoti kwa shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia mazingira, ripoti iliyoitwa *Global Green New Deal*, ambayo ilibeba tena fikra za 'uchumi wa kijani ' kwa jina la 'makubaliano mapya ya kijani'. Ripoti hii mpya kwa mara nyingine ilipendekeza matumizi ya

fedha za umma kuimarisha mtikisiko uliokuwa ukiukumba mfumo wa kibepari report kwenye ripoti mpya.

Notibuku yetu inaibuka toka nasaba tofauti, ambazo zimejikita katika Mkutano wa watu wa Ulimwengu wa Mabadiliko ya Tabia Nchi na Haki ya Mama Dunia (2010) na Mkutano wa Watu wa Ulimwengu wa Mabadiliko ya Tabia Nchi na Ulinzi wa Uhai (2015), yote ilifanyika Tiquipaya, Bolivia na kuendelea katika mikusanyiko kama Jukwaa la Maji na Dunia Mbadala (2018), Mkutano wa Watu (2017), na Jukwaa la Watu Kuhusu Asili (2020). Uelekeo huu ambao ulikua kutokana na mapambano ya wengi huko Marekani ya Ulatini, ni nidharia za, *buen vivir* na *teko porã* ('kuishi vema'). Badala ya kuuokoa *tu* ubepari,kitu ambacho ndio hasa mguso wa hoja za GND, hoja ya notibuku yetu ni kufikiri juu ya kubadili namna kuratibu jamii, kwa maneno mengine, kuboresha ufikiri juu ya ujenzi wa mfumo mpya. Kujenga fikra hizo, Ferdinandes anasema lazima kushirikishe vyama vya wafanyakazi ( vingiwavyo vikihofu juu ya suala la kupotea kwa ajira katika mchakato wa kuondoka kutoka ukaa kuelekea katika nishati-rejea) na vyama vya wakulima wadogo (vingiwavyo vikiwa vimeshikwa na hoja kuwa mjazano katika ardhi inaharibu asili na kutengeneza hali ya kutokuwepo usawa katika jamii).



Klay Kassem (Egypt), *The Mermaid Wedding*, 2021.

Tunapaswa kubadili mfumo, kama Ferdinand anavyojenga hoja, 'lakini hali ya kisiasa ya sasa si mujarabu kwa hili. Mrengo wa kulia upo imara katika nchi nyingi, hivyo ukanaji wa sayansi ya

tabia nchi upo mwingi vilevile'. Kwa hiyo, kwa haraka, mavuguvugu ya watu lazima yaweke agenda ya kuondoa nishati-ukaa mezani. Malengo manne yanatukabili:

1. **Kudhibiti maendeleo ya nchi za Magharibi**.
Huku kukiwa na idadi ya watu ambao ni chini ya 5% ya watu wote wa ulimwengu, Marekani inatumia theluthi ya karatasi zote zinazozalishwa duniani, takribani robo ya makaa ya mawe, takribani robo ya mafuta yote yanayozalishwa, na robo ya Alminium.
Sierra Club inasema kwamba katika Marekani ulaji/matumizi ya mtu mmoja ya 'nishati, metali, madini, mazao ya misitu, samaki, nafaka, nyama, na hata maji unadumaza ule wa watu wanaoishi nchi zinazoendelea'. Mataifa ya magharibi yanatakiwa yapunguze matumizi yao, na kuyarudisha nyuma, kama ambavyol Jason Hickel anavyoyaita, 'matumizi haribifu na yasiyo ya lazima' (kama vile nishati za fosili na viwanda vya silaha, na ndege za kibinafsi, uzalishaji wa viwandani wa nyama ya ng'ombe na falsafa ya jumla ya biashara isiyokuwa na mpango).
2. **Kujamiisha sekta muhimu za uzalishaji nishati.** Kukomesha ruzuku katika uzalishaji wa nishati zitokanazo na fosili na kuunda sekta ya nishati ya umma ambayo ipo katika msingi wa umalizaji mfumo wa nishati-ukaa.
3. **Kuifadhili Ajenda ya Kimataifa ya Tabia Nchi.** Kuhakikisha kwamba mataifa ya magharibi yanatimiza wajibu wake wa kihistoria kusaidia Mfuko wa Tabia Nchi ya Kijani, ambao utatumika kufadhili mageuzi yenye haki katika ulimwengu wa kusini.
4. **Kuiimarisha Sekta ya Umma.** Kujenga miundombinu zaidi kwaajili jamii badala ya kufanya hivyo kwaajili ya matumizi ya kibinafsi, mfano ujenzi zaidi we reli za kasi na mabasi ya umeme Ili kushusha matumizi ya magari ya binafsi. Nchi katika ulimwengu wa kusini zinapaswa kujenga uchumi wao wenyewe, ikiwamo kwa kutumia vema rasilimali zao wenyewe. Jambo lililopo hapa si suala kuzitumia rasilimali bali zawezaje kuvunwa na kutumika kwa maslahi ya jamii na maendeleo ya taifa badala ya ulimbikizaji kwa mabepari. Buen vivir – Ishi vema – maana yake kuweza kuvuka mpaka wa njaa na ufukara, kupata elimu na afya bora, ambavyo vitajengwa na sekta ya umma.

Hakuna sera ihusuyo masuala ya tabia nchi ambayo inaweza kukidhi ulimwengu mzima. Wale wenye kuzimeza rasilimali za dunia lazima wapunguze matumizi. Watu takribani bilioni mbili hawawezi kupata maji safi, ilhali nusu ya watu wote ulimwenguni hawamudu hawamudu kupata huduma bora ya afya. Maendeleo ya kijamii lazima yahakikishwe kwa wote, lakini maendeleo hayo lazima yajengwe katika uendelevu, ulio msingi wa usoshalisti.

Kwa huba,

Vijay

*Jarida hili limetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na,* **Muhemsi Mwakihwelo.** muhemsimwakihwelo@gmail.com